TASAF>> Imetekeleza mradi miaka mitano wilayani Karatu

Shule ya kisasa kijijini yawavutia wasichana

Na SULEIMAN JONGO

KUJENGWA shule mpya ya kisasa ya wasichana katika Kijiji cha Laja, Halmashauri ya Wilaya Karatu, mkoani Arusha, umeibua shangwe na kuwapa tumaini jipya wazazi na wanafunzi wa kijiji hicho na vijiji vya jirani.

Wakizungumza mbele ya uongozi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) uliofika kijijini hapo kutembelea shule hiyo iliyojengwa kupitia Mradi wa Kuondoa Umaskni Awamu ya Nne (TPRP IV), wananchi hao walisema mradi huo umewaokoa watoto hususan wa kike waliokuwa wakitembea umbali mrefu kufuata elimu katika vijiji jirani.

Akizungumzia shule hiyo, Christina Lucas, mkazi wa kijiji hicho alisema kabla ya kujengwa shule hiyo, wanafunzi hususan wasichana walikuwa wakiteseka kwa kutembea hadi kilometa nane kwenda katika kijiji kingine.

"Watoto wa kike ndiyo kundi lililokuwa linaathirika mno kwa sababu wanakutana na adha nyingi kama ujauzito wa lazima, hivyo kukatiza masomo yao.

"Kwa hiyo ilikuwa changamoto kubwa iliyowaathiri watoto wengi, baadhi walishindwa kumaliza kidato cha nne na kujikuta wakiacha masomo kutokana na kupata ujauzito.

"Shule hii imetusaidia mambo mengi, imepunguza utoro usiyo wa lazima kwa sababu mtoto akitoka nyumbani umbali wa kilometa nane njiani anakutana na changamoto nyingi, mara nyingine wanasindikizwa na bodaboda ambao baadhi ni hatari kwa usalama wa masomo yao," alisema.

Akizungumza kuhusu TASAF, Christina alipongeza na kushukuru Mradi wa Kupunguza Umaskini uliotekelezwa wilayani humo kwa miaka mitano na kufanikisha ujenzi wa miundombinu muhimu yakiwemo madaraja na shule hiyo.

"Tunaendelea kutoa maombi kwa sababu muhitaji hachoki kuomba, ni kweli tunayo mabweni pia tunahitaji maabara na nyumba zaidi za walimu kwa kuwa zilizopo hazitoshi.

"Tunatamani kama itawezekana Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kupitia TASAF atuone tena," alisema.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Laja, Daniel Panga, alipongeza juhudi zilizozaa shule hiyo hususan serikali chini ya Rais Dk. Samia kupitia TASAF na hivi sasa faida yake inaonekana.

"Baada ya shule kufunguliwa wazazi walikubaliana wanafunzi wote wakae hapa (shuleni) kwa sababu mara nyingi maeneo haya yamezungukwa na maporomoko, kipindi cha mvua inakuwa changamoto kubwa, kwani makorongo yanajaa maji na mtoto hawezi kupita," alisema.

Alisema wanafunzi hususan wasichana kukaa shuleni kumeleta tija kubwa ikiwemo kuwapa muda zaidi wa kujisomea.

"Wanafunzi kwa mazingira haya hawawezi kuzurura au kutoroka, tunawashukuru wanakijiji wa Laja kwa kazi nzuri ambayo wametusaidia. Maombi yetu ni kupatikana kwa maabara na kuongezwa nyumba za walimu," alisema Panga.

Akizungumza na wananchi waliokuwepo shuleni hapo, Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Shedrack Mziray, aliwapongeza kwa kazi nzuri waliyoifanya ambayo imekuwa na tija kubwa.

Mziray aliwasihi wananchi kuitunza shule hiyo na kuwahamasisha wananchi kuwapeleka shule watoto wao na kuwasimamia kikamilifu.

"Shule hii itakuwa na faida zaidi iwapo wanafunzi watasoma na kufaulu kwa kiwango kikubwa, huo utakuwa mwanzo wa kupata wataalamu wa fani mbalimbali nchini," alisema Mziray.

Uongozi wa TASAF ulitembelea wilayani Karatu kukagua baadhi ya miradi iliyotekelezwa kupitia mradi wa kupunguza umaskini uliofadhiliwa na Shirika la Nchi Zinazozalisha na Kuuza Mafuta kwa Wingi Duniani (OPEC).



SALAMU

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, akisalimiana na watoto, baada ya kushiriki Sala ya Ijumaa, katika Msikiti wa Alnassri, katika Kijiji cha Nanguji, Mkoa wa Kusini Pemba, jana. (Picha na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais).

JKCI kutibu moyo bila kufungua kifua

Na SUPERIUS ERNEST

MKURUGENZI wa Tiba za Moyo wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Tatizo Wami, amesema wanaendelea kujiimarisha katika huduma zao kwa kufanya upasuaji wa kubadilisha valvu za moyo bila kufungua kifua.

Amesema kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati, huduma hiyo inatolewa Tanzania pekee na inaokoa gharama kubwa za matibabu ya moyo ambayo ni ghali sana.

Wami ambaye ni daktari bingwa wa moyo, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati wa kambi ya siku moja ya upasuaji waliofanyiwa wagonjwa wawili kwa kuongozwa daktari mbobezi Nila Patel kutoka Mumbai nchini India aliyeshirikiana na jopo la madaktari wa JKCI.

"Huu ni upasuaji ambao asilimia kubwa unafanyika mgonjwa anapokuwa hawezi kufanyiwa upasuaji bila kufungua kifua, kwa hiyo wale wanaofanyiwa ni wenye umri mkubwa au wenye magonjwa zaidi ikiwemo moyo,"alisema.

Alisema kwa mgonjwa mmoja, matibabu hayo hugharimu hadi sh. milioni 100, kwani vifaa pekee ni sh. milioni 50 hadi 90 kulingana na aina ya mgonjwa na gharama za kufanya upasuaji ni sh. milioni nane.

"Upasuaji huu kwa nchi zilizoendelea unafanyika mara kwa mara, lakini kwa mwaka mmoja ambao tumefanya aina hii ya upasuaji ni wagonjwa wanane ambao tumefanikisha kuwafanyia matibabu ya aina hii,"alisema.

Alisema matibabu ya upasuaji huo ni ghali sana, kwasababu unahitaji vifaa maalumu ambavyo ni ghali, hivyo kufanikisha lazima kufanya maandalizi ya mgonjwa na kutambua aina ya vifaa anavyohitaji na kuviagiza nje ya nchi, ambapo inaweza kufika miezi sita ya matayarisho ya upasuaji.

Daktari huyo alisema matibabu hayo ni mwendelezo wa mpango wa huduma za kibingwa bobezi unaofadhiliwa na serikali kuwasaidia wananchi wasiokuwa na uwezo na kuokoa maisha yao.

Alieleza wagonjwa takriban asilimia 70 hadi 80, wanafadhiliwa na serikali na wachache ndiyo wenye uwezo wa kulipa gharama za matibabu hayo.

"Serikali imewezesha ununuzi wa vifaa vya utambuzi, kuongeza wataalamu bingwa ikiwemo, kuzibua matundu, viziba mishipa na mengineyo, huku akipongeza jitihada hizo za serikali kuwasaidia wananchi,"alisema.

Dk. Patel alisema amefurahi kufika JKCI kwa mara ya kwanza na kushirikiana na madaktari wa taasisi hiyo, kufanikisha upasuaji huo mgumu bila kufungua kifua.

Alisema amekuwa na uzoefu wa kufanya upasuaji zaidi ya miaka nane, huku akipongeza maendeleo ya JKCI na wataalamu wake katika kuendeleza upasuaji huo na kuokoa maisha ya wananchi hususan upasuaji huo unaofanyika kwa watu wazima kuanzia miaka 60 kuendelea.

MKUU WA IDARA

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara upasuaji wa tundu dogo wa JKCI, George Longopa, ambaye ni bingwa alisema kupitia kambi hiyo wamewafanyia upasuaji wagonjwa wawili kwa mafanikio.

Alieleza tangu kuanza kutoa huduma hizo wameweka kambi tatu wakishirikiana na madaktari bingwa kutoka nje ya nchi kwa lengo la kuwajengea uwezo zaidi katika upasuaji huo, ambapo wanafanya matibabu hayo kupitia mishipa ya mapajani badala ya kufungua kifua.

Longopa aliipongeza serikali inayoongozwa na Rais Dk. Samia kwa kuendelea kugharamia matibabu kwa wagonjwa hao, kwani bila hivyo isingewezekana kufanikisha hilo na kabla ya kufikia uwezo huo wagonjwa wengi walikuwa wakisafirishwa nje ya nchi jambo lililoigharimu fedha nyingi serikali.

MDAU WA VIFAA

Mdau wa ufadhili wa vifaa vya upasuaji wa moyo kupitia tundu dogo, Nelly Otenyo anayeishi Kenya, aliipongeza JKCI kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhakikisha wananchi wanapata matibabu ya moyo hususan ya upasuaji mgumu bila kufungua kifua.

"Nafurahi kuona upasuaji wa aina hii ukifanyika Tanzania, hivyo wagonjwa wa Afrika Mashariki na Kati wafike kutibiwa kwasababu zipo huduma za kibingwa zinazofanywa na madaktari bingwa wa hapa,"alisema.

Aliongeza wamekuwa wakishirikiana na hospitali nyingine Afrika ikiwemo ya JKCI huku akiwashukuru JKCI kwa ushirikiano wa karibu katika kuokoa maisha ya wananchi na kupunguza gharama za kusafirisha wagonjwa nje ya nchi.